

# MABANGO YAKUCHEKESHA

## *Utengenezaji usiofaa wa mabango*

Nilipokuwa nimetembelea Dubai, sikuweza kujizuia kwa kitu nilichokiona, ilikuwa jinsi bango lilivyokosewa kupachikwa. Kwa kuwa Kiarabu kimeandikwa kutoka kulia kwenda kushoto, inaonekana kama mtengenezaji

wa ishara alianza kutoka kulia na kukosa nafasi kushoto labda kwa sababu ya upangaji mbaya unaotokana na kutotumia vipimo sahihi. Mahali bango lilipo ni Nasser Square, katika jingo moja katikati ya mji wa Deira, Dubai.



Kinachoonekana hapa, kuna herufi 2 zilizobaki nje ya usawa wa eneo la jengo ambapo bango lilitahili kukaa sawa. **Inashangaza jinsi mteja na mmiliki wa jengo waliruhusu na kuvumilia kosa hili.**

***Sisi Sign Industries Ltd, mabango yetu yote hutengenezwa kwa umakini na kufuata viwango vya kimataifa, na hakuna nafasi kabisa ya kosa kama hili.***